

SHULE YA SEKONDARI KIMWERI

P.O BOX 433
KOROGWE-TANGA
TANZANIA

TAR:.....

KUMB.NA.SSK/FI/AD/52/VOL.1/23

JINA LA MWANAFUNZI:.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIMWERI WILAYA YA KOROGWE MKOA WA TANGA MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya **SEKONDARI KIMWERI** kwa mwaka wa masomo 2021. Nakupongeza kwa kupata bahati hii na nina imani utatumia nafasi hii vizuri kwa manufaa yako wewe mwenyewe na kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 na unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 ndani ya siku 14.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 Sare za shule:

- i) Rangi ya uniform ni kitambaa kizito cha maruni (damu yamzee) wasichana washone sketi zenye rinda box na marinda mawili pembeni. Wavulana suruali zenye marinda mawili na pindo la kukunja. Sketi 2, mashati 2, suruali 2, (kwa maelekezo zaidi wasiliana na uongozi wa shule Kwa namba 0712016273/0719406705/0747004003)
- ii) Wanafunzi wote wa kike washone sketi ndefu zinazofika kwenye kiwiko cha miguu (sketi inayofunika soksi) na wanaovaa hijabu hawaruhusiwi kuvaa suruali.
- iii) Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba, vya ngozi na vyenye kisigino kifupi jozi mbili.
- iv) Jozi mbili soksi nyeupe kwa wasichana na fupi nyeusi kwa wavulana.
- v) Rangi ya sweta ni maruni yenye V mbele.

2.2 Vifaa vya shule

- i) Mwanafunzi anatakiwa kuwa na daftari 10 (counter books) na madaftari madogo 10.
- ii) Mathematical set
- iii) Kalamu za kuandikia, rula na penseli.
- iv) Ndoo ndogo ya lita kumi na fagio la chelewa.

3.0 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:


- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Utoro sugu.
- e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- f) Kupigana au kupiga
- g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- h) Kudharau bendera ya Taifa
- i) Kuwa mjamzito/kupata mimba/ kusababisha mimba.
- j) Kuoja au kuolewa
- k) Kutoa mimba
- l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- m) Kukataa adhabu kwa makusudi
- n) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:

- a) Medical Examination Form' ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara atakapo ripoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzina mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU KATIKA SHULE HII.


..... HEADMISTRESS
KIMWERI SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 433, KOROGWE

KIAMBATANISHO "B"
SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA KIMWERI
FOMU YA KUKUBALI NAFASI ULIOPEWA

SEHEMU A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI (ijazwe na mwanafunzi)

1. Jina kamili:.....
2. Tarehe ya kuzaliwa:.....
3. Mahali ulipozaliwa mji/kijiji:.....
4. Mahali unapoishi sasa hivi:.....

KUKUBALI NAFASI (ijazwe na mwanafunzi)

Mimiambaye maelezo yangu ni haya hapo juu, nimesoma maagizo yaliyoagizwa na katii sheria za shule.

Naahidi kwamba niwapo shuleni nitajitahidi kuzingatia maelezo yote yanayotolewa mara kwa mara na walezi wangu ili kupata taaluma bora na maadili yanayotakiwa.

Sahihi ya mwanafunzi:.....

Tarehe:.....

SEHEMU B: TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI (ijazwe na mzazi/mlezi)

1. Jina kamili:
2. Mzazi/mlezi wa:.....
3. Kazi:
4. Mahali anapoishi:
5. Anuani:Namba ya simu:
6. Sahihi ya mzazi/mlezi:.....
7. Tarehe:

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

KIMWERI SEKONDARY SCHOOL

P. O. BOX 433

KOROGWE

REQUEST MEDICAL EXAMINATION

The medical officer

.....

.....

.....

Student:.....

Please examine the above as to his/her physical and mental for full time schooling under the listed categories.

.....

HEADMISTRESS

MEDICAL EXAMINATION REQUEST

I have examine the above student named and consider him/her physical and mentally fit/unfit for school time course.

1. Eyesight.

2. Hearing:

3. Limbs:

4. Speech.

5. Venereal disease

6. Leprosy

7. Epilepsy

8. Pregnancy

Date Signature: